



**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR  
KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS IKULU**

Nambari ya Simu: 2230814/5

**S. L. P. 2422,**

Nambari ya Fax: 2233722

**ZANZIBAR - TANZANIA**

06 Agosti, 2021

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi leo ameungana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mh. Samia Suluhu Hassan na viongozi mbalimbali wa Kitaifa katika Ibada ya kuuaga na kutoa heshima za mwisho kwa mwili wa Marehemu Elias John Kwandikwa aliyekuwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Tukio lililofanyika Katika viwanja vya Karimjee, Jijini Dar es Salaam.

Dkt. Mwinyi amemzungumzia Marehemu Kwandikwa kama kiongozi aliyekuwa wa Mfano na Kielelezo cha Uongozi bora huku akisema Taifa limegubikwa na Majonzi makubwa.

Akimzungumzia Marehemu, Rais Dkt. Mwinyi alisema Katika Uhai wake, Marehemu Kwandikwa alikuwa Waziri wa Kwanza Kumtembelea Ikulu Zanzibar kwaajili ya Kujitambulisha na kwa hakika walifanya kazi kwa karibu sana.

Rais Dkt. Mwinyi alimuelezea Marehemu kwa umahiri wake kwa kusema “*Marehemu alionyesha umahiri na Uadilifu Mkubwa katika kutekeleza majukumu yake kwa Nafasi mbalimbali alizopewa dhamana ya kuziongoza. Juhudi na Tabia zake ziliwavutia sana viongozi wetu wa juu wa Chama cha Mapinduzi na Serikali, Na Hatimaye Rais wa Awamu wa tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Marehemu John Pombe Magufuli alimua kukitumia Ipasavyo kipaji chake Uwezo na Uzoefu aliokuwa nao kwa kumpa majukumu mazito zaidi ya Kitaifa kwa kumchagua kuwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchuzi na Mawasiliano mwezi Oktoba mwaka 2017..*” Alisema Rais Dkt. Mwinyi.

Aliongeza kwa Kusema, “*Daima tutamkumbuka kwa mchango wake, katika kuimarisha Ulinzi wa Taifa letu na Kudumisha hali ya Amani na Utulivu.*”